


KOROSHO



MKL
SB401
.C3
K67


**SOKOINE
NATIONAL
AGRICUTURAL
LIBRARY**



**KWA NJIA ZOTE HIZO MBILI, SHAMBA
LAZIMA LIWE LIMETAYARISHWA KAMA
MWEZI MMOJAKABLAMSIMU WA MVUA
HAUJAANZA.**




**MBEGU WATUMIAZO NI ZILE ZILIZOTOKA
KWENYE MITI ILIYO NA AFYA NZURI**



064917 8

**BAADA YA KUVUNA MBEGU KUTOKA
MITI BORA HUCHUKUA NDOO YENYE
MAJI NAKUTUMBUKIZA MBEGU ZOTE.
NYINGINE HUELEA JUU, NYINGINE
HUZAMA CHINI. ZILE ZINAZOZAMA NI
NZITO ZENYE AFYA NA NDIZO MBEGU
HASA ZINAZOFAA KUPANDWA.**




NJIA YA KWANZA INAFAA NA MBEGU HUPANDWA MBILI AU TATU KATIKA SHIMO MOJA. KILA SHIMO LIWE UMBALI WA FUTU 38 AU HATUA 17 KUTOKA JINGINE ILI MIMEA IWEZE KUISHI VIZURI PASIPO KUGOMBEA CHAKULA ARDHINI.




KAMA MBEGU ZIMEPANDWA KATIKA SHIMO, ZIPANDWE UMBALI WA SENTIMETA 23 AU INCHI 9 KATIKA PEMBE TATU AU PIMA UREFU WA UNYAYO.

**SOKOINE
NATIONAL
AGRICUTURAL
LIBRARY**

UNAPOCHIMBA MASHIMO, WEKA UDONGO JUU MBALI NA UDONGO WA CHINI. PIMA MASHIMO NYAYO MBILI UPANA NA UREFU.





CHANGANYA UDONGO WA JUU NA SAMADI, HALAFU TANGULIZA CHINI YA SHIMO. BAADAE JAZIA UDONGO ULIOTOKA CHINI YA SHIMO.



**WAKATI MIMBA INAKUA, MATAWI YA
CHINI HUKATWA KUUWEZESHA MTI
UKUE WIMA NA KUWA WENYE NGUVU,
MTU NI LAZIMA AWEZE KUTEMBEA
CHINI YAMTI. MATAWI YA CHINI KABISA
YAKIWA JUU KIDOGO YA KICHWA
CHAKE.**



**UDONGO MNYEVU HUTUMIWA KUHIFADHI
MAHALI PALIPOKATWA.**




**KAMA TAWI MOJA LITAPATA UGONJWA,
NI LAZIMA LIKATWE KWA MSUMENO
HARAKA NA KUCHOMWA NJE KABISA
YA SHAMBA KABLA UGONJWA
HAUJAENEA KATIKA MTI MZIMA AU
MITI ILIYO KARIBU.**




**WANAKIJIJI HUWEKA SHAMBA KATIKA
HALI YA USAFI. HII NI MUHIMU SANA,
WANAKATA MAGUGU YOTE KWA
KUTUMIA KWANJA AU PANGA.**



MATUNDA YAKIIVIA MTINI, HUANGUKA YENYEWWE CHINI NA NDIPO WANAKIJIJI HUYAOKOTA. HAWATIKISI MITI AU KUYAANGUA MABIBO YALIYOIVA. KIJIJI KIZIMA KINASAIIDIA KATIKA KUVUNA MAZAO. SHAMBA NI SAFI NA NI RAHISI KUKUSANYA MAZAO.



**SIKU HATA SIKU MABIBO HUKUSANYWA
NA KOROSHO KUONDOLEWA NA
KUWEKWA PAMOJA KWENYE MATAWI
YALIYOTENGENEZA KIJIJINI. KOROSHO
ZILIZOOZA NA ZISIZO NA KITU
HUTUPWA. MAWE, MCHANGA NA
MAJANI HUTOLEWA.**




USIWEKE KOROSHO KARIBU NA UKUTA.




**WAZEZA KUPATA HASARA KAMA
KOROSHO ZITAHARIBIWA NA MAPANYA.**



**ZUIA WADUDU NA MAPANYA WAHARIBIFU
KWA KUZIBA MASHIMO.**



**JENGA KICHANJA NA HALAFU WEKA
MAGUNIA JUU YAKE.**



**UKIFUATA NJIA BORA ZA KILIMO,
UTAONGEZA MAZAO YAKO AMBAYO
YATAKULETEA FAIDA KUBWA.**

MKL 26 201